# Dhima ya Viambishi Ngeli za Nomino za Ki-Vunjo

*Ruth Ndekiro*
*Chuo Kikuu cha Ghana*

**Ikisiri**

**Makala haya yanashughulikia dhima ya viambishi ngeli za nomino za ki-Vunjo. Utafiti kuhusu makala haya ulifanyika Kaskazini Mashariki mwa Tanzania mkoani Kilimanjaro katika wilaya ya Moshi Vijijini. Mbinu ya Usampulishaji Nasibu Pangilifu ilitumika katika utafiti huu katika kupanga umri na jinsi, ambapo jinsi ya kike wamehusika watoa taarifa 15 na jinsi ya kiume wamehusika watoa taarifa 15. Watoa taarifa wote 30 walikuwa wazungumzaji wa ki-Vunjo wenye umri kati ya miaka 44-74. Taarifa zimekusanywa kwa watoa taarifa kwa kutumia njia za hojaji, usaili na ushuhudiaji. Utafiti huu ulilenga kubainisha dhima ya viambishi ngeli za ki-Vunjo. Ili kutimiza lengo hili, Mkabala wa Kisemantiki ulitumika sambamba na Nadharia ya Mofolojia Asilia (NMA) iliyopendekezwa na Dressler (1985) na Wurzel (1987). Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa lugha ya ki-Vunjo ina idadi ya ngeli 18 ambapo imebainika kuwa katika viambishi ngeli kuna dhima mbalimbali zinazojitokeza zaidi ya umoja na wingi. Dhima hizo ni: ukubwa, udogo, uzuri na ubaya. Mwisho, utafiti huu umetoa mapendekezo ya tafiti fuatishi.**

**Maneno Muhimu:** Dhima, Viambishi, Nomino, Semantiki

**Utangulizi**

Utafiti mwingi umefanywa kuhusu lugha za Kibantu. Kuna utafiti unaofafanua lugha hizo kwa ujumla na mwingine unaohusu vipengele mahususi. Hata hivyo, inaonekana wazi kwamba lugha nyingine za Kibantu kama vile ki-Vunjo hazijachunguzwa au zimeshughulikiwa kwa kiwango cha chini katika vipengele fulani. Nurse na Phillippson (2003:4) wanadai kuwa lugha za Kibantu hazijashughulikiwa sana. Wanaeleza kuwa lugha chache sana zina sarufi inayoeleweka, ilhali nyingine zina orodha ya msamiati tu.

Kuna wataalamu mbalimbali waliowahi kufanya utafiti juu ya "ngeli" katika lugha mbalimbali. Miongoni mwao ni pamoja na Polome (1976), na Kihore na wenzake (2003) ambao wametumia kigezo cha kimofolojia katika uainishaji wa ngeli za nomino za Kiswahili. Kwa kutumia kigezo hiki, wataalamu hao wameainisha ngeli 18 za Kiswahili. Idadi ya ngeli 18 katika uainishaji wa nomino umeainishwa pia na Kahigi (2005) ijapokuwa katika uainishaji wake anatumia Mkabala wa Viambishi Awali vya Nomino huku hasa akijikita katika lugha ya si-Sumbwa.

Mohammed (2001:41–52) naye ameainisha ngeli katika lugha ya Kiswahili. Kwa kutumia Mkabala wa Kisemantiki, uchambuzi wake unaelezea aina za nomino zinazobebwa na kila ngeli. Anaeleza kuwa katika ngeli ya Ki-/Vi- mbali na kubeba nomino za vitu visivyo na uhai, pia ina nomino chache zinazohusu wanyama na watu (uk 42) kwa mfano, 'kifaru/vifaru', 'kiboko/viboko', 'kijana/vijana' na 'kiongozi/ viongozi'.

Kihore na wenzake (2001) wanaona kuwa kwa kutumia kigezo walichokiita msingi wa kutumia Kiambishi cha Nomino na Kiambishi cha Upatanishi wa Kisarufi, uainishaji utakuwa timilifu zaidi. Hata hivyo, wanaeleza kuwa bado kuna tatizo la muainisho mdogo wa ngeli. Aidha, wanaeleza kuwa muainisho huu unatokana na kuwapo kwa nomino ambazo ingawa hubeba kiambishi ngeli cha ngeli fulani, huweza kuchukua upatanisho wa kisarufi wa ngeli nyingine tofauti. Tukiwanukuu wanaeleza kuwa:

> *Nomino zinazohusu majina ya watu, wanyama, ndege, samaki, na viumbe wa aina yake huweza kuwa na viambishi vya nomino za ngeli nyingine lakini bado ukachukua viambishi vya upatanishi wa kisarufi wa ngeli za 1 na 2 (A – WA -)* (uk. 109).

Swali la kujiuliza ni je, muainisho mdogo katika lugha ya ki-Vunjo ukoje? Swali hili limeshughulikiwa katika utafiti huu.

Viambishi awali vya ngeli za nomino huweza kubeba dhima nyingine zaidi ya dhima ya umoja na wingi kama vile dhima ya udogo, ukubwa, uzuri au ubaya. Wataalamu mbalimbali kama vile Ashton (1944), Gibbe (1983a) na Maho (1999) wameeleza dhima hizo. Kwa mfano, Ashton (kashatajwa) anaainisha ngeli za nomino katika lugha ya Kiswahili kwa kutumia Mkabala wa Jozi ya Viambishi vya Nomino vya Umoja na Wingi kuunda ngeli moja. Pia, alieleza kuwa kuna viambishi awali vya nomino vichache vinavyoweza kuonesha dhima ya ukubwa na udogo katika ngeli. Kwa mfano, //ki-// anaeleza kuwa inaweza kuonesha udogo katika baadhi ya ngeli lakini hakuzitaja ni ngeli zipi.

Polome (1976: 94-95) tofauti na Ashton (1944) anaainisha ngeli za nomino katika lugha ya Kiswahili kwa kutumia Mkabala wa Viambishi Awali vya Nomino, ambapo kila kiambishi anakipa ngeli yake. Kutokana na uinishaji huo, alipata jumla ya ngeli 18 za Kiswahili. Aidha, katika uainishaji huo, Polome (kishatajwa) anaeleza dhima ya ukubwa na kuonesha inapatikana katika ngeli ya tano, mfano ni nomino kama jitu, jisu na toto. Vilevile, ameonesha dhima ya udogo ya kiambishi //ki-// katika ngeli ya 7 ambapo ameeleza kuwa katika Mame-Bantu ilikuwa Ka-. Swali tulilojiuliza ni kuwa hali kama hii inajitokeza katika nomino za lugha ya ki-Vunjo?

Gibbe (1983a) anaendeleza mjadala huu kwa kuongeza kuwa kiambishi //ki-// kinaweza kubeba dhima nyingi, ambazo ni: kudunisha, udogo uliokithiri, kawaida, dhiki, penzi na kadhalika. Wazo hili linaungwa mkono na Mohammed (2001: 41-52) anapoeleza kuwa kiambishi ngeli //ki-// katika kazi mbalimbali za kisarufi zilizotangulia kimeelezwa kuwa kina dhima ya kuonesha udogo. Zaidi, anaona kuwa pia kina dhima nyingine tofauti na hiyo. Anaeleza kuwa kiambishi //ki-// wakati mwingine huwa na dhima ya kukuza na kusisitiza. Kwa mfano:

(a) Nilikiona kijua[1] njiani

(b) Alitokwa na kijasho[2]

Katika mifano hii, kiambishi //ki-// katika maneno ‘kijua’ na ‘kijasho’ hakina dhima ya udogo badala yake kina dhima ya kuonesha kukuzwa kwa nomino ‘jua’ na ‘jasho’.

Kwa upande wake Kahigi (2005: 117) anaainisha ngeli za nomino za lugha ya si-Sumbwa kwa Mkabala wa Viambishi Awali vya Nomino na Upatanishi wa Kisarufi ambapo alipata ngeli 18. Kahigi (keshatajwa) anaeleza kuwa dhima ya ukubwa na udogo inajitokeza katika ngeli za nomino fuatizi. Kwa kuongezea, anaeleza kuwa upo uwezekano wa dhima hizi kujitokeza katika nomino nyingine, na pia hata katika ngeli nyingine. Anahitimisha kuwa kuna haja ya kufanya utafiti wa kina juu ya tofauti za maumbo ya ukubwa na udogo ili kujua kama yanatokana na tofauti za kisemantiki au sababu nyingine kama vile lahaja.

Akitofautiana na Kahigi (keshatajwa), Mwendamseke (2011) anaeleza kuwa katika lugha ya Kibena huwa kuna baadhi ya viambishi vya msingi ambavyo huwa na dhima ya udogo. Vilevile, dhima ya ukubwa, uzuri na ubaya, hupatikana katika ngeli ya 5 na 6. Kwa maelezo haya, ni dhahiri kuwa dhima zinazobebwa na viambishi ngeli si lazima zijitokeze katika nomino fuatizi.

Japokuwa lugha za Kibantu zina mfumo wa ngeli, kuna tofauti fulanifulani zinazojitokeza miongoni mwa lugha hizo (Maho 1999). Hata hivyo, uchunguzi wa kina kuhusu dhima ya viambishi ngeli za nomino katika lugha ya ki-Vunjo haujafanyika kabisa. Hivyo, utafiti huu unakusudia kufafanua dhima mbalimbali zinazojitokeza katika viambishi ngeli vya nomino za ki-Vunjo ili kuziba pengo lililopo katika suala la dhima za viambishi ngeli za ki-Kivunjo.

**Msingi wa Kinadharia**

Utafiti huu uliongozwa na misingi ya nadharia mbili: Nadharia ya Mofolojia Asili (NMA) na Mkabala wa Kisemantiki.

[1] Kijua imetumika kwa maana ya ‘scorching sun’

[2] Kijasho imetumika kwa maana ya ‘excessive sweat’

**Kiunzi cha Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Mofolojia Asilia (NMA) iliyopendekezwa na Dressler (1985) na Wurzel (1987). Nadharia hii iliongoza utafiti huu kuainisha ngeli za nomino za lugha ya ki-Vunjo kisemantiki. Dressler (keshatajwa) na Wurzel (keshatajwa) wanadai kuwa kuna uhusiano wa mofimu na maana zake katika neno. Wurzel (keshatajwa) anakubaliana na Dressler (keshatajwa) kwa kudai kuwa Nadharia ya Mofolojia Asilia (NMA) inachambua uhusiano baina ya umbo na maana. Maelezo haya yalituongoza kubaini mofimu za nomino za lugha ya ki-Vunjo na maana zake. Hivyo, maelezo haya yalitusaidia kuzipanga nomino hizo kwa kuzingatia dhima zake. Aidha, katika utafiti huu, tulitumia Mkabala wa Kisemantiki. Mikabala hiyo ilitumika sambamba na Nadharia ya Mofolojia Asilia ili kukidhi malengo ya utafiti huu.

**Mkabala wa Kisemantiki**

Mkabala wa Kisemantiki ni utaratibu unaotumika kuzigawa nomino za lugha za Kibantu kwa kuangalia uhusiano wa nomino hizo kimaana. Nomino zenye maana moja zinawekwa katika kundi moja la ngeli. Katika mkabala huu, wanazuoni wengi wa mitalaa ya sarufi za lugha za Kibantu wanakubaliana kwamba hapo zamani mgawanyiko wa ngeli za nomino ulijikita katika msingi wa maana. Kwa msingi huo, nomino zenye kiunzi fulani cha maana inayoziunganisha huwekwa katika ngeli moja. Baadhi ya wanazuoni hao ni Whiteley (1961) na Dixon (1968) katika (Abayo, 2003). Hivyo, nomino zenye kiunzi fulani cha maana inayoziunganisha huwekwa katika ngeli moja.

Udhaifu wa mkabala huu unatokana na ukweli kwamba maana hubadilika. Massamba (1995) na Kihore na wenzake (2003) wanaeleza kwamba tatizo kubwa kabisa la kigezo hiki ni kule kubadilikabadilika kwa maana za maneno kutokana na mazingira ya kijiografia na mabadiliko ya utamaduni. Kwa hivyo, ni vigumu kukitumia kigezo hiki pasi na utata. Kutokana na utata unaojitokeza, wataalamu wengi wameonelea kuwa ni bora kutokitumia kigezo hiki kama msingi mkuu wa uainishaji ngeli. Hata hivyo, umuhimu wa mkabala huu wa kisemantiki katika utafiti huu ulionekana pale ambapo tulikuwa tunashughulikia muainisho mdogo wa nomino za ki-Vunjo.

**Methodolojia**

Utafiti kuhusu makala haya ulifanyika Kaskazini Mashariki mwa Tanzania mkoani Kilimanjaro katika wilaya ya Moshi Vijijini. Usampulishaji Nasibu Pangilifu ulitumika katika kupanga umri na jinsi, ambapo jinsi ya kike walihusika watoa taarifa 15 na jinsi ya kiume walihusika watoa taarifa 15. Watoa taarifa wote 30 walikuwa wazungumzaji wa ki-Vunjo wenye umri kati ya miaka 44-74. Vilevile, utafiti huu ulitumia data zilizotokana na hojaji, usaili na ushuhudiaji. Katika kuchakata hojaji, mtafiti aligawa hojaji zilizokuwa na maswali yaliyolenga kupata data kuhusu nomino mbalimbali za ki-Vunjo katika maumbo yake ya umoja na wingi, kwa watoa taarifa 20 ambapo hojaji 18 zilirudishwa zikiwa zimejazwa. Kwa kutumia njia ya ushuhudiaji, mtafiti alienda wilaya ya Moshi Vijijini na alishiriki katika mazungumzo mbalimbali na watoa taarifa. Wakati wa mazungumzo, alirekodi mazungumzo hayo kwa njia vinasa sauti na shajara. Katika usaili, mtafiti alihojiana ana kwa ana na watoa taarifa 10. Njia zote tatu zilimuwezesha mtafiti kukusanya data nyingi zinazohusu nomino za aina mbalimbali zikionesha muainisho wake mdogo kimaana. Hivyo, matumizi ya mbinu mbalimbali za ukusanyaji data yalisaidia kupata data za kweli, sahihi na za kutosha kadiri ya malengo ya utafiti huu. Mathalani, mkabala mseto yaani, mkabala wa takwimu na mkabala wa maelezo ulitumika katika uwasilishaji na uchambuzi wa data ya utafiti kuhusu makala haya. Vilevile, data zilizokuwa katika lugha ya ki-Vunjo zilitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili.

**Matokeo ya Utafiti**

Data ifuatayo katika Jedwali Na.1 hapa chini ni baadhi ya mifano ya nomino mbalimbali za ki-Vunjo katika maumbo yake ya umoja na wingi zilizokusanywa na mtafiti kwa njia ya hojaji, usaili na ushuhudiaji, ambapo baadhi ya watoa taarifa waliweza kutaja nomino mbalimbali za ki-Vunjo katika maumbo yake ya umoja na wingi. Kimsingi, nomino hizo alizozibaini mtafiti kupitia njia hizi tatu za hojaji, usaili na ushuhudiaji, zilitumika kuchambua, kufafanua na dhima mbalimbali za viambishi ngeli za nomino katika sehemu inayofuata ya uchambuzi wa data:

**Jadweli Na.1: Nomino Mbalimbali za ki-Vunjo katika Maumbo yake ya Umoja na Wingi**

| Na. | Nomino katika Umoja | Nomino katika Wingi |
|---|---|---|
| 1 | Mfee 'Mzazi' | Wafee 'Wazazi' |
| 2 | Mchili 'Msimamizi' | Wachili 'Wasimamizi' |
| 3 | Mndu 'Mtu' | Wandu 'Watu' |
| 4 | Mkori 'Mpishi' | Wakori 'Wapishi' |
| 5 | Øpapa 'Baba' | Øpapa 'Baba' |
| 6 | Ølawutanyi 'Shemeji' | Ølawutanyi 'Shemeji' |
| 7 | Ømamela 'Kilembwe' | Ømamela 'Kilembwe' |
| 8 | Imuembe 'Embe' | Miembe 'Miembe' |
| 49 | Imukepe 'Kopo' | Mikepe 'Makopo' |
| 10 | Imukoke 'Mchwa' | Mikoke 'Mchwa' |
| 11 | Mři 'Mti' | Mři 'Mti' |
| 12 | Mtsu 'Moshi' | M Tsu 'Moshi' |
| 13 | Mtsiri 'Mkaa' | Mtsiri 'Mkaa' |
| 14 | Iwenje 'Mende' | Iwenje 'Mende' |
| 15 | Mawenje 'Mende' | Mawenje 'Mende' |
| 16 | Ipfue 'Nyani' | Ipfue 'Nyani' |
| 17 | Kikapu 'Kikapu' | Shikapu 'Vikapu' |
| 18 | Kimiyo 'Kidole' | Shimiyo 'Vidole' |
| 19 | Kitara 'Kitanda' | Shitara 'Vitanda' |
| 20 | Kyela 'Chakula' | Shyela 'Vyakula' |
| 21 | Kyeri 'Wakati' | Shyeri 'Wakati' |
| 22 | Kyaro 'Safari' | Shyaro 'Safari' |
| 23 | Ndaa 'Chawa' | Ndaa 'Chawa' |
| 24 | Ndeu 'Tumbo' | Ndeu 'Tumbo' |
| 25 | Numba 'Nyumba' | Numba 'Nyumba' |
| 26 | Mbeu 'Mbegu' | Mbeu 'Mbegu' |
| 27 | Mbeta 'Ndege' | Mbeta 'Ndege' |
| 28 | Urusu 'Uzi' | Urusu 'Uzi' |
| 29 | Ndusu 'Nyuzi' | Ndusu 'Nyuzi' |
| 30 | Unjui 'Unywele' | Njui 'Nywele' |
| 31 | Njaa 'Kucha' | Njaa 'Kucha' |
| 32 | Unjaa 'Ukucha' | Unjaa 'Ukucha' |
| 33 | Upoi 'Fimbo ya kutembelea' | Upoi 'Fimbo ya kutembelea' |
| 34 | Ngyupoi 'Fimbo za kutembelea' | Ngyupoi 'Fimbo za kutembelea' |
| 35 | Iyewo 'Jino' | Mayewo 'Meno' |
| 35 | Iwee 'Ziwa' | Mawee 'Maziwa' |
| 37 | Kiliko 'Kijiko' | Shiliko 'Vijiko' |
| 38 | Numba 'Nyumba' | Numba 'Nyumba' |
| 39 | Urusu 'Uzi' | Ndusu 'Nyuzi' |
| 40 | Uwicho 'Ubaya' | Mawicho 'Mabaya' |
| 41 | Kuřende 'Mguu' | Mařende 'Miguu' |
| 42 | Kuwokonyi 'Mkononi' | Mawokonyi 'Mikononi' |
| 43 | Hafanyi 'Pachafu' | Kufanyi 'Pachafu' |

| | | |
|---|---|---|
| 44 | Hala | ‘Pale’ |
| 45 | Kula | ‘Kule’ |
| 46 | Iřema | ‘Kulima’ |
| 47 | Handu ‘Mahali’ | Kundu ‘Mahali’ |
| 48 | Kiṟinyi ‘Chumbani’ | Shiṟinyi ‘Vyumbani’ |
| 49 | Ṟema ‘Shamba’ | Maṟema ‘Mashamba’ |
| 50 | Ṟemenyi ‘Shambani’ | Maṟemenyi ‘Mashambani’ |

Baada ya uchunguzi na uchambuzi wa data kuhusu nomino za aina mbalimbali za ki-Vunjo pamoja na maumbo yake ya umoja na wingi zilizokusanywa uwandani kama zilivyobainishwa katika Jedwali Na.1 hapo juu, sehemu hii inafafanua na kuainisha kila ngeli ya nomino kwa kuonesha viambishi ngeli vyake.

**Dhima za KNg katika Lugha ya ki-Vunjo**

Licha ya viambishi ngeli katika lugha za ki-Vunjo kuwa na dhima ya kuonesha umoja na wingi, pia baadhi ya viambishi hivyo huwa na dhima ya ukubwa na udogo tangu enzi ya Mame-Bantu. Wataalamu mbalimbali kama vile Ashton (1944), Maho (1999), Harjula (ht) na Kahigi (2005) katika kazi zao wameeleza kuhusu dhima za ukubwa na udogo kama ilivyoelezwa katika kipengele cha x

Nomino za lugha ya ki-Vunjo zilizotumika katika utafiti huu zinaonesha kuwa viambishi ngeli vina dhima nyingine mbali ya dhima za ukubwa na udogo. Dhima nyingine za viambishi ngeli kwa mujibu wa data iliyotumika ni udhaifu, uzuri, ubaya, wembamba, ufupi, tabia mbaya na tabia nzuri. Dhima za udogo, uzuri, ufupi, udhaifu, wembamba na tabia nzuri hupatikana katika ngeli ya 7 na 8. Dhima ya ukubwa, ubaya, urefu na tabia mbaya hupatikana katika ngeli ya 5 na 6.

Data iliyokusanywa kutoka uwandani imedhihirisha kuwa dhima zinazobebwa na kiambishi ngeli (kuanzia sasa KNg) katika nomino za ki-Vunjo ni zaidi ya dhima za ukubwa, udogo, umoja na wingi. Pia data hiyo imedhihirisha kuwa dhima hizo zimetawanyika katika ngeli tofauti kama maelezo yafuatayo yanavyoonesha:

**Dhima ya Ukubwa na Ubaya**

Dhima ya ukubwa na ubaya katika ngeli za nomino za lugha ya ki-Vunjo zinajidhihirisha katika ngeli ya 5 na 6 wingi yenye viambishi //i-// na //ma-//. Dhima hizo hujidhihirisha kwa shina la nomino kutoka ngeli nyingine kuhamishiwa katika ngeli ya 5 na 6 kwa kuambikwa viambishi //i-// umoja na //ma-// wingi. Nomino inayopatikana baada ya shina kuambikwa viambishi hivyo hubeba dhima zilizotajwa. Katika baadhi ya lugha za Kibantu kama vile Kisisumbwa, Kirunyambo, Kiswahili na Kibena, dhima ya ukubwa na ubaya hubebwa na viambishi vya umoja na wingi vya ngeli moja. Kwa mfano, katika lugha ya Kibena dhima ya ukubwa na ubaya hupatikana katika ngeli ya 5 na 6 ambayo huwakilishwa na viambishi //li-// umoja na //ma-// wingi ambavyo kwa kutumia mkabala wa Jozi ya Viambishi vya Umoja na Wingi ni ngeli moja. Viambishi vyenye dhima ya ukubwa na ubaya katika nomino za ki-Vunjo vinaoneshwa katika Jedwali Na.2 hapo chini:

**Jedwali Na.2: Dhima ya Ukubwa na Ubaya katika Ngeli ya 5 na 6**

| Na | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (a) | itosho ‘chungu kikubwa’ | matosho ‘vyungu vikubwa’ |
| (b) | iwařo ‘ua kubwa’ | mawařo ‘mauwa makubwa’ |
| (c) | ipata ‘kata kubwa’ | mapata ‘kata kubwa’ |

**Dhima za Udogo, Udhaifu na Ubaya**

Dhima ya udogo, udhaifu na ubaya katika ngeli za nomino za ki-Vunjo hupatikana katika ngeli ya 7 na 8 inayowakilishwa na viambishi //ki-// na //shi-//. Dhima hizo hujidhihirisha kwa shina la nomino kutoka ngeli nyingine kuhamishiwa katika ngeli ya 7 na 8 kwa kuambikwa viambishi //ki-// umoja na //shi-// wingi. Nomino inayopatikana baada ya shina kuambikwa viambishi hivyo hubeba dhima zilizotajwa. Dhima zote zinaambatana katika viambishi hivyo. Ili kujua ni dhima ipi inahusika kwa wakati fulani inategemea muktadha uliopo kwa wakati huo. Dhima hizo zinajidhihirisha katika Jedwali Na.3 kama ifuatavyo:

**Jedwali Na.3: Dhima ya Udogo, Udhaifu na Ubaya**

| Na. | Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|---|
| (a) | kimana | 'kitoto kigonjwa' | shiwana | 'vitoto vigonywa' |
| (b) | kimřo | 'kichwa kidogo' | shimřo | 'vichwa vidogo' |
| (c) | kipfumu | 'kimkuki kibaya' | shipfumu | 'vimikuki kibaya' |
| (d) | kinguruche | 'kikata kibaya' | shinguruche | 'vikata kibaya' |

**Dhima za Udogo, Uzuri, Ufupi, Urefu na Wembamba**

Dhima za udogo, uzuri, ufupi, urefu na wembamba katika ngeli za nomino za lugha ya ki-Vunjo zinapatikana katika ngeli ya 7 na 8. Katika ngeli hiyo, si nomino zote zinazopangwa hubeba dhima hizo. Ngeli ya 7 na 8 pia huchukua nomino ambazo zimepatikana kwa kuhamisha mashina ya nomino zinazopatikana katika ngeli nyingine kwa kuambikwa viambishi //ki-// umoja na //shi-// wingi. Dhima hizo hujidhihirisha katika nomino za ki-Vunjo kama zinavyooneshwa katika Jedwali Na.4 hapo chini:

**Jedwali Na.4: Dhima za Udogo, Uzuri, Urefu, Ufupi na Wembamba**

| Na. | Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|---|
| (a) | kiřende | 'mguu mdogo' | shiřende | 'miguu midogo' |
| (b) | kiwoko | 'mkono mzuri' | shiwoko | 'mikono mizuri' |
| (c) | kiwařo | 'ua zuri' | shiwařo | 'maua mazuri' |

**Dhima ya Tabia Mbaya na Tabia Nzuri**

Katika nomino za lugha ya ki-Vunjo KNg kinabeba pia dhima ya tabia mbaya na tabia nzuri. Dhima hizi zimetengwa peke yake japo zinabebwa na viambishi ambavyo vinabeba dhima nyingine kwa sababu zinahusu viumbe hisivu tu, yaani binadamu na wanyama wanaofugwa kama vile mbwa na paka. Dhima ya tabia mbaya inapatikana katika ngeli ya 5 na 6 ambayo inawakilishwa na viambishi //i-/ Ø// na //ma-// na dhima ya tabia nzuri inapatikana katika ngeli ya 7 na 8 ambayo huwakilishwa na viambishi //ki-// na //shi-//. Binadamu na wanyama wanapokuwa na tabia mbaya hudunishwa kwa kufananishwa na vitu visivyo hisivu. Kutokana na hali hiyo mashina ya nomino zinazohusu viumbe hivyo huambikwa kiambishi //i-// umoja na //ma-// wingi ili binadamu na wanyama hao waonekane wamedunishwa. Binadamu na wanyama wenye tabia nzuri hawadunishwi bali huoneshwa kuwa ni wazuri kwa mashina ya nomino zao kuambikwa kiambishi //ki-// umoja na //shi-// wingi. Yafuatayo ni maelezo ya mtoa taarifa akieleza kuhusu dhima ya tabia mbaya na tabia nzuri katika nomino za ki-Vunjo:

> *Watu na wanyama wanaofugwa kama vile mbwa na paka kama wana tabia mbaya majina yao hudunishwa kwa majina yao kufananishwa na majina ya vitu visivyo hai ambavyo havina uwezo wa kutenda wala kufikiri jambo lolote. Kama watu na wanyama wana tabia nzuri hawadunishwi bali huoneshwa kuwa ni wazuri kwa nomino zao kusemwa kwa uzuri* (Ezra Kombe 2013).

Kutokana na dondoo la mtoa taarifa huyo, ni wazi kuwa dhima ya tabia mbaya inahusishwa na binadamu na wanyama wafugwao ambao wanategemewa kuwa na tabia nzuri lakini wanakuwa na tabia mbaya. Hivyo, binadamu na wanyama hao huonwa na jamii kuwa hawana tofauti na viumbe visivyoweza kuwaza au kujua zuri na baya kwa asili au kwa kufundishwa. Binadamu na wanyama wenye tabia nzuri huoneshwa kuwa ni wazuri kwa nomino zao kusemwa kwa uzuri. Zingatia mifano ifuatayo katika Jedwali Na. 5 na Na.6.

**Jedwali Na.5: Dhima ya Tabia Mbaya katika Ngeli ya 5 na 6**

| Na. | Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|---|
| (a) | imana | 'litoto' | mawana | 'mitoto' |
| (b) | ikite | 'kambwa' | makite | 'mambwa' |
| (c) | imbafu | 'jambazi' | mambafu | 'majambazi' |

**Jedwali Na.6: Dhima ya Tabia Nzuri katika Ngeli ya 7 na 8**

| Na. | Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|---|
| (a) | kisichana | 'msichana mwenye tabia nzuri' | shisichana | 'wasichana wenye tabia nzuri' |
| (b) | kipaka | 'paka mwenye tabia nzuri' | shipaka | 'paka wenye tabia nzuri' |
| (c) | kimana | 'mtoto mwenye tabia nzuri' | shimana | 'watoto wenye tabia nzuri' |

Kama uchanganuzi wa data kuhusu dhima za viambishi ngeli katika nomino za lugha ya ki-Vunjo unavyoonesha hapo juu, ni dhahiri kuwa dhima zinazobebwa na KNg katika lugha za Kibantu zimetawanyika katika ngeli za nomino mbalimbali. Wataalamu mbalimbali wameeleza upatikanaji wa dhima za viambishi ngeli za nomino katika lugha za Kibantu. Maelezo ya wataalamu hao yametofautiana kwa mfano, Maho (1999) anaeleza kuwa katika lugha za Kibantu dhima ya udogo inapatikana katika ngeli ya 12, 19 na kwa kiasi kidogo katika ngeli ya 11. Aidha, anaeleza kuwa dhima ya ukubwa inapatikana katika ngeli ya 5 na 7, na kwa kiasi kidogo katika ngeli ya 20. Kahigi (2005) anatofautiana na Maho (keshatajwa) anapoeleza kuwa katika ngeli za nomino za Kirunyambo dhima ya udogo inapatikana katika ngeli ya 12 na 13 tu na dhima ya ukubwa inapatikana katika ngeli ya 5 na 6 tu.

Vilevile, uchanganuzi wa data za nomino za ki-Vunjo umeonesha kuwa dhima zinazojidhihirisha katika KNg si ukubwa na udogo tu, bali kuna dhima nyingine kama vile uzuri, ubaya, urefu, wembamba, udhaifu, tabia nzuri na tabia mbaya. Dhima hizo zimetawanyika katika ngeli tofautitofauti kwa mfano, ukubwa, ubaya na tabia mbaya hupatikana katika ngeli ya 5 na 6. Dhima za udogo, udhaifu, uzuri, ufupi, urefu, wembamba na tabia nzuri hupatikana katika ngeli ya 7 na 8.

Utokeaji wa dhima hizo katika ngeli za nomino za ki-Vunjo una changamoto kwa sababu dhima hizo hujidhihirisha vilevile katika viambishi vilevile. Hii ina maana kwamba kiambishi kimoja katika nomino za ki-Vunjo kina uwezo wa kubeba dhima zaidi ya moja kwa wakati mmoja. Katika hali kama hiyo, ili kujua kiambishi hicho kina dhima gani ni lazima nomino hiyo iwe katika tungo na iambatane na maneno mengine hususani vivumishi ndipo utaelewa ni dhima gani inabebwa na kiambishi husika. Kwa mfano, kiambishi //ki-// huweza kuwa na dhima zaidi ya moja kama inavyothibitishwa na mifano ifuatayo katika Jedwali Na.7.

**Jedwali Na.7: Dhima za Udogo, Uzuri, Ufupi, Urefu, Tabia Nzuri na Wembamba**

| Na. | Tungo Zenye Nomino na Vivumishi | | Dhima |
|---|---|---|---|
| i | kimana kitutu | 'katoto kadogo' | udogo |
| ii | kimana kicha | 'katoto kazuri' | uzuri |
| iii | kimana kifuhi | 'katoto kafupi' | ufupi |
| iv | kimana kileshi | 'katoto karefu' | urefu |
| v | kimana kisuse | 'katoto kembamba' | wembamba |
| vi | kimana kirawari | 'katoto hodari' | tabia nzuri |

Kwa hivyo, suala la dhima zinazobebwa na KNg katika nomino za ki-Vunjo lina changamoto. Changamoto hiyo ni namna ya kutambua dhima inayobebwa na KNg kama nomino haijatumika sambamba na kivumishi. Changamoto hii inatokana na ukweli kuwa KNg kimoja cha nomino za ki-Vunjo hubeba dhima zaidi ya moja. Pia, kuna viambishi awali ngeli ambavyo kuna wakati huwa na dhima ya kuonesha umoja na wingi tu, lakini viambishi hivyo hivyo wakati mwingine hubeba dhima ya umoja na wingi pamoja na dhima nyingine kama vile udogo, uzuri, ufupi, wembamba, urefu na tabia nzuri kama inavyojidhihirisha katika Jedwali Na.7.

### Hitimisho

Utafiti huu umeonesha kuwa katika viambishi ngeli kuna dhima mbalimbali zinazojitokeza zaidi ya umoja na wingi. Dhima hizo ni: ukubwa, udogo, uzuri na ubaya, ambapo dhima ya ukubwa, uzuri na ubaya zimebainika katika ngeli ya 5/6 na dhima ya udogo, uzuri na ubaya zimebainika katika ngeli ya 12/13 na ngeli ya 7/8. Matokeo haya yanatofautiana kidogo na hali ilivyo kwenye baadhi ya lugha

nyingine za Kibantu. Kwa mfano, katika lugha ya Ki-Runyambo dhima ya udogo ipo katika ngeli ya 12/14 peke yake (Kahigi, 2005). Pia, dhima ya ubaya inapatikana katika viambishi vya nomino zinazohusu binadamu na wanyama wanaofugwa na binadamu tu, kama tulivyoeleza katika kipengele 4.1.3. Hivyo, utafiti huu umeonesha dhima hizi kwa ujumla hazina budi kuwekwa bayana ili kueleweka kwa wazungumzaji husika kwa sababu kiambishi kimoja kina uwezo wa kuwa na dhima zaidi ya moja. Hivyo, utata hauna budi uondolewe ili kuweza kueleweka katika mazungumzo.

**Mapendekezo ya Tafiti Fuatishi**

Utafiti huu umeshughulikia uainishaji wa ngeli za nomino za lugha ya ki-Vunjo kisemantiki na kuainisha dhima zake tu. Katika utafiti huu haikuwezekana kushughulikia kila kitu kinachohusu uainishaji wa ngeli za nomino katika lugha ya ki-Vunjo. Kuna Vipengele vingine vya kiisimu ambavyo vilikuwa nje ya mawanda ya utafiti huu lakini ni muhimu vifanyiwe utafiti. Vipengele hivyo ni: mosi, uainishaji wa ngeli za nomino za lugha ya ki-Vunjo kwa vigezo vingine kama vile kigezo cha kisintaksia. Pili, ulinganishaji wa kiisimu na kihistoria wa ngeli za nomino za ki-Vunjo na lugha nyingine zilizo jirani nayo. Tatu, uchunguzi wa kina kuhusu mabadiliko ya ngeli yaliyotokea tangu enzi za Mame-Bantu katika lugha ya ki-Vunjo na athari za nomino za kigeni katika ngeli za nomino za lugha hii.

Utafiti katika maeneo yaliyotajwa hapo juu ni muhimu sana kufanyika kwa sababu hamna tafiti za kina zilizofanywa kuhusu maeneo hayo. Tafiti za kina katika maeneo hayo zitatoa mchango mkubwa kwa kuhifadhi taarifa mbalimbali na kuandika uchambuzi wa kisarufi wa lugha ya ki-Vunjo. Pia, tafiti katika maeneo hayo zitatoa mchango wa maarifa katika uwanja wa taaluma za lugha kwa ujumla.

**Marejeleo**

Abayo, A. (2003). "Swahili Noun Class Systeam: A Critical Survey of the Loan Words". Tasnifu ya Umahiri. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ashton, E. O. (1944). *Swahili Grammar: Including intonatio.* London: Longman Group Ltd.

Dressler, W. U. (1985). On the Predictiveness of Natural Morphology. Journal of Linguistics 21, pag 321-338.

Gibbe, A. G. (1983a). "Uchambuzi wa Nomino za Ngeli ya Kwanza Katika Kiswahili". Katika TUKI, *Lugha ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI, uk 244 – 256.

Harjula, L. (2013). (ht). The Ha Noun Class System Revisited. http://www.linguistics.fi/julkaisut/SKY2006.1/1.3.3.HARJULA.pdf. Imepakuliwa tarehe 10/04/2013.

John, B. (2011. Nafasi ya Viarudhi katika Lugha ya ki-Vunjo; Uamilifu wa Toni katika Irabu Ndefu na Fupi. Tasnifu ya Umahiri Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kahigi, K. K. (2005). "The Sisumbwa Noun: It's Classes and Derivation", in *Occasional Paper In Linguistics*. Dar es Salaam: LOT.

Kihore, Y. M. na wenzake (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu, (SAMAKISA).* Dar es Salaam, TUKI.

Maho, J. (1999). "A Comparative Study of Bantu Noun Classes". Goteborg Universty, Unpublished PhD Dissertation.

Massamba, D. P. B. (1995). "The Classification of Ci-Ruri Nouns", katika *Journal of Asian and African Studies,* Nos.48-49. ILCAA, Tokyo University of Foreign Studies.

Mohammed, M. A. (2001). *Modern Swahili Grammar*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd

Mwendamseke, F. J. (2011). Uainishaji wa Ngeli za Nomino katika Lugha ya Kibena. MA haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nurse, D. na Philippson, G. (2003). The Bantu Languages of East Africa: Lexicostatistical Survey. Katika E.Polome na C.P. Hill (eds) *Language in Tanzania.* O.U.P, London.

Polome, E. C. (1976). *Swahili Language Handbook*. Washington, D.C, Center for Applied Linguistics.